## Godline William Mangilima, (1965–2007)

Godline William Mangilima alikuwa mchungaji na msimamizi wa kanisa kutoka Tanzania.

### Maisha ya zamani

Godline William Mangilima alizaliwa Bunda, Mkoa wa Mara, nchini Tanzania, Juni 25, 1965, na wazazi wake walikuwa Augustine na Hellena Mangilima. Alitumia maisha yake ya utotoni katika Mji wa Bunda, ambao wakati huo ulikuwa ukiimarika kiuchumi na kuwavutia watu wengi wa imani tofauti za kidini. Inasemekana kwamba alipokuwa akipita kwenye stendi ya mabasi, aliona bango kubwa lenye picha ya mhubiri, lakini hakuelewa. Aliposogea mbele mita chache tu, alikutana na mtu yule ambaye alikuwa ameona picha yake kwenye bango. Alifurahi sana na kuamua kumfuata mtu huyo, na kujikuta akihudhuria mkutano mkubwa wa injili wa Waadventista. Mkutano ulipoisha jioni ya siku hiyo ya kwanza aliazimia kurudi tena siku iliyofuata. Mwishoni mwa mfululizo huo aliamua kujiunga na Kanisa la Waadventista Wasabato, na akabatizwa Desemba 13, 1980. Alikuwa na umri wa miaka 15 tu wakati alipokuwa amebatizwa.

### Elimu

Godline Mangilima alisoma Shule ya Msingi ya Mugaja. Alifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na kuwa mwanafunzi wa kwanza kabisa kuhudhuria shule ya sekondari kutokea shule hiyo ya msingi. Kulikuwa na shule chache sana za sekondari Mkoani Mara wakati huo. Baadaye alijiunga na Shule ya Sekondari ya Kilimo ya Kilosa iliyopo Morogoro, na kuhitimu Elimu ya Ngazi ya Kawaida mwaka 1988. Wakati huo wanafunzi waliosoma shule za ufundi walipaswa kujiunga na shule ya Ufundi Moshi au Chuo cha Ufundi Mbeya. Alichaguliwa kujiunga na Chuo cha Ufundi Mbeya kwa Cheti cha Ufundi Kamili mwaka 1993. Mwaka 2001 hadi 2004 alisoma shahada ya Theolojia, na kuhitimu mwaka 2004.

### Uchungaji na Kifo

Mangilima akiwa Mbeya alikutana na mchungaji aitwaye Anyitike Mwaipopo kwenye mkutano wa Makambi ya Mbeya. Kulikuwa na uamsho mkubwa katika mkutano huo wa makambi, na wito ulipotolewa kwa wale ambao wangependa kujiunga na huduma ya uchungaji, mara moja Godline aliitikia wito wa kumtumikia Mungu kama mchungaji. Akikumbuka tukio hili, Mchungaji Mwaipopo anasema, “Nilipokutana na mvulana huyo mdogo nilimwona mchungaji ndani yake. Nilimuona kiongozi aliyejaa hekima na aliye tayari kumtumikia Mungu, kwa hiyo niliwasiliana mara moja na Mzee Simon Bukuku, aliyekuwa katibu-mhazini wa Fildi ya Kusini Magharibi mwa Tanzania, na baada ya mahojiano, Godline aliitwa na kutumwa katika mtaa wa Mbozi wenye kujaa changamoto nyingi.” Mangilima alihudumu hapo kuanzia mwaka 1993 hadi 1995. Mwaka 1996 alihudumu katika Mtaa wa Mbalizi kwa muda wa mwaka mmoja, na kisha Iringa mwaka 1997 hadi 2003. Kisha akatumikia Fildi ya Kusini Magharibi mwa

Tanzania kama mkurugenzi wa Idara ya Vijana (2003-2005). Mwaka 2004 alichaguliwa kuwa katibu mtendaji wa South West Tanzania Field, nafasi ambayo aliitumikia hadi alipofariki kwa ajali ya gari mwaka 2007.

**Urithi Aliotuachia**

Mangilima anakumbukwa kwa utumishi wake wa kipekee na wa kujitoa, uliowatia moyo vijana wengi kujiunga na mafunzo ya Kiongozi Mkuu (Master Guide) na kujiunga na huduma uchungaji. Pia anakumbukwa kwa uwezo wake wa kuleta umoja pale palipokuwa na mifarakano, kama vile alipokuwa akichunga mtaa mgumu wa Mbozi, Sumbawanga na Tunduma.